# MAELEZO YA KURANI KUHUSU GIZA CHINI YA BAHARI NA MAWIMBI YA NDANI

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Maelezo ya Kurani kuhusu maisha katika bahari ya kina, na giza ndani yake, na jinsi inathibitisha matokeo ya kisayansi ya kisasa.

**Aina:** Makala Ushahidi Uislamu Ni Ukweli Miujiza ya Kisayansi ya Kurani Tukufu

**Na:** islam-guide.com


**Iliyochapishwa mnamo:** 23 Nov 2021
**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 27 Feb 2023

Mungu anasema katika Kurani:

***“Au (vitendo vya makafiri) ni kama giza katika bahari kuu, iliyo funikiwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia asiuone...” (Kurani 24:40)***




Aya hii inataja giza linalopatikana katika majimakuu, ambapo mtu akinyosha mkono wake, hawezi kuiona. Giza chini ya bahari huanza karibu na kina cha mita 200 kuenda chini. Kwa kina hiki, takriban hakuna mwanga.(angalia picha ya 1). Chini ya kina cha mita 1000 hakuna mwanga kabisa. [1] Binadamu hawawezi kupiga mbizi zaidi ya mita arobaini bila msaada wa manowari au vifaa maalum. Binadamu hawawezi kuishi bila msaada katika sehemu ya giza ya bahari, kama vile kwa kina cha mita 200.




Picha 1: Kati ya asilimia 3 na 30 ya mwanga wa jua hurudishwa kutoka juu ya bahari. Kisha karibu rangi zote saba za wigo wa mwanga hupotea moja kwa moja katika mita 200 za kwanza, isipokuwa mwanga wa buluu. (*Bahari*, Elder na Pernetta, uk. 27)

Wanasayansi hivi karibuni wamegundua giza hili kwa kutumia vifaa maalum na nyambizi ambazo zimewawezesha kufikia kina cha bahari.

Pia tunaweza kuelewa kutokana na sentensi zifuatazo katika aya iliyopita, **“...katika bahari kuu, iliyo funikiwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu....”**, kwamba maji ya kina ya bahari yanafunikwa na mawimbi, na juu ya mawimbi haya ni mawimbi mengine. Ni wazi kwamba aina ya pili ya mawimbi ni mawimbi ya juu tunayoyaona, kwa sababu aya inataja kuwa juu ya mawimbi ya aina ya pili kuna mawingu. Lakini mawimbi ya kwanza ni yapi? Wanasayansi hivi karibuni wamegundua kwamba kuna mawimbi ya ndani ambayo “hutokea kwenye mipaka ya wiani kati ya tabaka za wiani tofauti.” [2] (angalia picha ya 2).




Picha ya 2: Mawimbi ya ndani katika mpaka kati ya tabaka mbili za maji ya wiani tofauti. Moja ni zito (ya chini), nyingine uzito wake ni ndogo (ya juu). (Uchunguzi wa bahari, Jumla, uk. 204.)

Mawimbi ya ndani yanafunika maji ya kina ya bahari kwa sababu maji ya kina yana wiani mkubwa kuliko maji yaliyo juu yao. Mawimbi ya ndani huwa kama mawimbi ya juu. Yanaweza pia kuvuma, kama mawimbi ya juu. Mawimbi ya ndani hayawezi kuonekana kwa jicho la mwanadamu, lakini yanaweza kugunduliwa kwa kuchambua halijoto au mabadiliko ya kiwango cha chumvi katika mahali fulani.[3]

---

## Rejeo la maelezo:


| | |
|---|---|
| [1] | *Bahari, Elder and Pernetta, uk. 27.* |
| [2] | *Uchunguzi wa bahari, Jumla, uk. 205.* |
| [3] | *Uchunguzi wa bahari*, Jumla, uk. 205. |


Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://webcache001.islamreligion.com/sw/articles/217/maelezo-ya-kurani-kuhusu-giza-chini-ya-bahari-na-mawimbi-ya-ndani

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2026 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.